# Upimaji wa uoni na usikivu kwa watoto wenye umri wa shule
Jumbe muhimu: Usikivu na afya ya kusika kwa watoto

## Somo la kwanza: Usikivu kwa watoto

Watoto wenye upungufu wa usikivu hupata shida kusikia na kutambua sauti. Watoto wanaweza kuwa na matatizo ya usikivu ya viwango tofauti, kuanzia kiwango kidogo hadi kikubwa sana. Mtoto mwenye upungufu wa usikivu wa kiwango kidogo hawezi kusikia vizuri kama watoto wengine. Mtoto mwenye upungufu mkubwa sana wa usikivu katika masikio yote mawili anaweza kuwa na usikivu hafifu sana au asiweze kusikia kabisa. Hali hii hujulikana kama “ukiziwi”

Matatizo mengi ya usikivu yanaweza kuzuiwa, kutibiwa au kudhibitiwa kwa kutumia vifaa saidizi vya kusikia na/ au ukarabati.

## Somo la pili: Afya ya masikio

Ili kusikia vizuri, ni lazima sehemu zote za sikio ziwe na afya njema na zifanye kazi ipasavyo. Wakati wa upimaji, ni muhimu kukagua nje na ndani ya sikio.

Kutambua masikio yenye afya bora namna yanavyoonekana na kujua dalili za matatizo ya kiafya ya masikio ni muhimu kwa ajili ya upimaji wa milango ya fahamu. Matatizo ya kiafya ya masikio yanaweza kusababishwa na:


- Masikio yaliyoziba
- Maambukizi ya masikio
- Hatari zitokanazo na mtindo wa maisha na mazingira.

**Tahadhari**

Ni muhimu kubainisha matatizo ya afya ya masikio mapema. Yasipotibiwa, matatizo haya yanaweza kusababisha hitaji la upasuaji na uharibifu wa kudumu wa sikio

**Dalili za masikio yenye afya njema.**

| Sehemu ya sikio | Dalili za afya | Picha |
|---|---|---|
| **Pinna (Sehemu ya nje ya sikio)** | • Hakuna dalili za kuharibika/ kuumia, uvimbe, kutokwa na uchafu au kubadilika kwa rangi.<br>• Sehemu ya nje ya sikio ipo |  |
| **Njia ya sikio** | • Njiia ya sikio ipo<br>• Njia ya sikio haijaziba<br>• Hakuna uvimbe wala wekundu | |

| | | |
|---|---|---|
| **Ngoma ya sikio** | • ·Ni safi na inang'aa kiasi (inaonesha upande wa ndani kidogo)<br>• Rangi nyeupe au kijivu-lulu<br>• Hakuna matobo. |  |

## Somo la tatu: Maandalizi ya upimaji

### Kabla ya siku ya upimaji

| Hatua ya | Kazi | Picha |
|---|---|---|
| **1. Kagua vifaa** | Hakikisha una vifaa vyote vinavyohitajika na kama vinafanya kazi vizuri,<br>Vifaa hivyo nipamoja na:<br>• Odiomita<br>• Hedifoni<br>• Otoskopi. |  |

### Siku ya upimaji

| Hatua ya | Kazi | Picha |
|---|---|---|
| **1. Andaa eneo la upimaji** | Panga vizuri meza, viti, na vifaa kwa ajili ya upimaji wa masikio na usikivu. Hakikisha eneo lina ukimya wa kutosha (hakuna kelele nyingi za nje) |  |
| **2. Tayarisha watoto kwa ajili ya kufanya upimaji** | Elezea upimaji kwa watoto na waonyeshe vifaa vya kufanya upimaji |  |

## Somo la nne: Upimaji wa Usikivu na afya ya sikio

Fomu ya upimaji itakusaidia wakati wa upimaji wa usikivu na afya ya sikio kwa kila mtoto, kurekodi matokeo na kupanga mpango wa kumsaidia kulingana na mahitaji yake.

Kama mtoto atakamilisha upimaji wa uoni kwanza, ridhaa yake na majibu ya maswali ya awali yatakuwa yamekwisha kurekodiwa

### Upimaji wa Usikivu

Upimaji wa uwezo wa kusikia unafanywa kwa kutumia kifaa kinachoitwa Audiomita. Wakati wa upimaji, mtoto atasikiliza sauti kupitia hedifoni na ataashiria anazoweza kuzisikia.

### Fanya mazoezi kuhusu upimaji wa kusikia

Hakikisha mtoto anaelewa utaratibu wa kupima kwa kufanya mazoezi nao kwanza.

1. Weka kiwango cha masafa ya sauti kama 1000Hz, na sauti kwenye 40dB.

2. Kwa kuanza na sikio la kulia, muulize mtoto kama anasikia sauti yoyote
3. Andika matokeo

| Matokeo | Kazi |
|---|---|
| Kama mtoto atajibu | Andika **'Ndiyo'**kama jibu na endelea. |
| Kama mtoto hataweza kujibu baada ya majaribio matatu | Andika **Hapana kama jibu na** endelea na upimaji wa afya ya masikio. |

Endelea na upimaji kamili iwapo tu mtoto atapata 'Ndiyo' kwa masikio yote mawili

**Namna ya kufanya upimaji wa kusikia**

Mchakato wa kufanya upimaji wa kusikia umeelezewa kwenye orodha ya mambo ya kuzingatia wakati wa upimaji

Masikio yote mawili yanapimwa Usikivu kwenye:

- 1000Hz na 20dB
- 2000Hz na 20dB
- 4000Hz na 20dB.

| Hatua za upimaji wa kusikia | Picha |
|---|---|
| 1. Anza na sikio la kulia. Weka masafa ya sauti 1000Hz<br>2. Wasilisha sauti mara tatu<br>3. Andika chini kama mtoto anaweza au hawezi kusikia sauti<br>4. Rudia hatua ya 2-3 kwa kila masafa.<br>5. Rudia mchakato wote kwa sikio la kushoto. |  |

| Matokeo | Kazi |
|---|---|
| Kama atakuwa na alama mbili au zaidi kwa kila masafa kwa masikio yote mawili | **Amefaulu** |
| Chini ya alama mbili kwa masafa yoyote kwa sikio lolote | ☞ **Mpe rufaa** kwenda kwa mtaalamu wa afya ya masikio |

**Kukagua afya ya kila sikio**

Ili kukagua sikio la mtoto:

1. Mara zote nawa na kausha mikono yako kwa sabuni au sanitaizakabla na baada ya ya kila ukaguzi wa sikio utakaoufanya.
2. Tumia otoskopi kuangalia kwa karibu nje na ndani ya sikio.
3. Rekodi matokeo kwa kutumia fomu ya upimaji

| Matokeo | Kazi |
|---|---|
| Masikio yote yana afya njema | Rekodi maatokeo na **endelea** |

| | |
|---|---|
| Sikio mojawapo au masikio yote mawili hayana afya njema. | ☞ **Mpe mtoto rufaa** kwamtaalamu wa masikio na uandike sababu |

## Panga

Baada ya kukamilisha upimaji wa uoni na usikivu, andika mpango utakaoutumia

| Matokeo | Kazi |
|---|---|
| **Hakuhudhuria** | Iwapo mtoto hayupo siku ya upimaji, jaza sehemu ya“ Hakuhudhuria” kwenye fomu ya mpango na weka alama ya tiki kwenye sehemu ya 'panga upimaji tena'. |
| **Amefaulu matokeo yote** | Chagua 'Amefaulu matokeo yote'kwenye sehemu ya mpango iwapomtoto amepata matokeo ya 'Amefaulu' kwa vipimo vyote hivi:<br>• Upimaji wauoni<br>• Upimaji waafya ya macho<br>• Upimaji wausikivu<br>• Upimaji wa afya ya masikio |
| **Matokeo ya 'Rufaa' kwa kipimo chochote** | Jadili na mzazi/mlezi umuhimu wa kumpa mtoto ☞ Rufaa iwapo atapata matokeo ya ☞ Rufaa kwa kipimo chochote kati ya hivi vifuatavyo:<br>• Maswali ya awali kabla ya kufanya vipimo<br>• Upimaji wa uoni<br>• Upimaji wa afya ya macho<br>• Upimajiwa usikivu<br>• Upimaji wa afya ya masikio |
| **Mzazi/mlezi ana wasiwasi** | Ikiwa mtoto amepata matokeo ya 'Amefaulu' na mzazi/mlezi wake alikuwa na wasiwasi kuhusu uoni au usikivu wa mtoto kwenye maswali ya awali:<br>• Jadili matokeo ya vipimo pamoja na mzazi/mlezi<br>• Mwelezekuwa mtoto amefaulu upimaji wa uoni na usikivuna mpe fursa ya kufanyiwa upimaji tena ndani ya mwezi mmoja. |
| **Mtoto tayari ana miwani au vifaa saidizi vya kusikia** | Ikiwa mtoto ambaye tayari anatumia miwani au vifaa saidizi vya kusikia atapata matokeo ya ☞ Rufaa mshauri mzazi/mlezi ampeleke mtoto kwa mtaalamu anayemhudumia |
| **Orodha yaufuatiliaji wa rufaa** | Mratibu wa shule anapaswa kuandika taarifa za kila mtoto aliyepata matokeo ya ☞ Rufaa kwenye orodha ya ufuatiliaji, na kumkabidhi orodha hiyo mratibu mkuu wa upimaji. |